

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'

Simu Na. 027-2530022
Barua pepe:ded@hanangdc.go.tz

Tovuti:www.hanangdc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Hanang',
2 Barabara ya Amani,
S.L.P. 2,
27382 Ganana – Hanang',
MANYARA.

TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI YA UPANGISHAJI WA KANTINI YA HALMASHAURI YA WILAYA

ZABUNI NA.LGA/059/2023/2024/NC/02

Tarehe: 26/04/2023

KWA: WAZABUNI WOTE

1. Mwaliko huu wa Zabuni unatokana na Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' kwa Mwaka 2023/2024 wa fedha unaoonekana katika TANEPS.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' inapenda kualika zabuni kutoka kwa mtu binafsi, makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kutoa huduma ya chakula katika Kantini mbalimbali kutuma maombi yao kwa Zabuni hii.
3. Unakaribishwa kuwasilisha Zabuni (Bei) kwa ajili ya utoaji huduma kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika **Sehemu ya Pili**.
4. Mwombaji asiwe Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' au Mheshimiwa Diwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'.
5. Mwombaji wa zabuni ataje bei ya Kupanga kantini kwa Mwezi/mwaka.

6. Mwombaji atakayefanikiwa atatakiwa kuweka dhamana ya asilimia 10% ya thamani ya Mkataba.
7. Mwombaji asiwe na deni lolote katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'.
8. Zabuni zote zijazwe kikamilifu kwa kuainisha Namba ya Zabuni LGA/059/2023/2024/NC/02 ya Upangishaji wa Kantini ya Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' na kuiwasilisha kupitia TANEPS.
9. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Zabuni ni **11/05/2023** kabla ya *saa 5:00* Asubuh. Zabuni zitafunguliwa kupitia TANEPS katika tovuti: www.taneps.go.tz.
10. Zabuni ambazo hazijawasilishwa kupitia TANEPS au zilizowasilisha katika muundo usiokubalika na TANEPS hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini bila kujali mazingira yoyote yale.



Ibrahim E. Mbogo
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'

MKURUGENZI MTE...
HAL MASHAURI YA WILAYA YA
HANANG